**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA IRINGA**
**NYERERE HIGH SCHOOL - MIGOLI**


**Namba za simu**

Mkuu wa shule **0767072036/0625943568**

Makamu mkuu wa shule **0752 160 384**
Taaluma **0 7 4 6 9 0 1 0 1 1 / 0 7 5 2 4 4 8 6 7**

Malezi **0762994887/0620597926**

Mhasibu **0755 834 274**

**S.L.P.**

**240,**

**IRINGA.**


JINA LA MWANAFUNZI ________________________________

S.L.P ____________

__________________

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO SHULE YA SEKONDARI NYERERE HIGH SCHOOL-MIGOLI HALMASHAURI YA WILAYA YA IRINGA, MKOA WA IRINGA KWA MWAKA 2023/2024.**

## 1.0 UTANGULIZI

Kwa niaba ya Jumuiya ya **Nyerere High School-migoli**, napenda kuchukua nafasi hii kukupongeza kwa kuchaguliwa kwako kujiunga na shule yetu. Kuchaguliwa kwako kumezingatia mafanikio uliyoyapata katika kumaliza elimu ya kidato cha Nne na matokeo yako mazuri katika mtihani wa Taifa. Shule hii inapokea wanafunzi mchanganyiko wa kutwa kwa kidato cha I hadi IV na bweni kwa kidato cha V na VI ambao ni wavulana tu. Hata hivyo zipo nafasi chache za hostel kwa kidato cha I- IV. Nafasi hizo hutolewa kwa wale tu wenye shida ya mahali pa kuishi hapa Migoli. Michepuo inayofundishwa katika shule hii kwa kidato cha tano ni, **HGL, HGK, HKL, EGM** na **HGE**.

Shule yetu itafunguliwa tarehe **14.08.2023. M**wanafunzi atapaswa kuripoti tarehe **13.08.2023** na mwisho wa kuripoti ni tarehe **31.08.2023** Siku ya kuripoti utatakiwa kufika shuleni na kusajiliwa tayari kwa masomo. Wakati wa kusajiliwa utatakiwa kulipa ada ya shule na kuthibitisha kuwa umetimiza masharti mengine yote kama inavyoonesha katika barua hii. Jaza fomu zote zilizoambatanishwa na uje nazo na kukabidhi wakati wa kusajiliwa. Michepuo inayofundishwa katika shule hii kwa kidato cha tano na cha sita ni, **HGL, HGK, HKL, EGM** na **HGE**.

## 1. 1 MAHALI SHULE ILIPO

**Nyerere High School-Migoli** ipo kijiji cha **Migoli** Halmashauri ya **Wilaya ya Iringa.**
Kwa kutokea **Iringa mjini**, shule ipo umbali wa **km 92** barabara ya **Iringa-Dodoma** katika kijiji cha **Migoli.** Vilevile kwa upande wa kutokea **Dodoma jiji**, shule ipo umbali wa **km 162** barabaraya **Dodoma - Iringa** katika kijiji cha **Migoli.**

### 1.2 Usafiri

Usafiri wa basi kutoka **Iringa** unapatikana stendi kuu ya zamani ya mabasi **Iringa-Mjini** na stendikuu mpya ya mabasi ya **Mkoa wa Iringa** iliyopo **Igumbilo**. Nauli yake ni Tsh **5,000/-**
Usafiri wa basi kutoka **Dodoma** unapatikana stendi ya mabasi ya **Mkoa wa Dodoma** iliyopo **Nanenane**. Nauli yake ni Tsh **10,000/-** Kituo cha kushukia ni **Migoli**

**Karibu sana Nyerere High School-Migoli, nakutakia safari njema ya kuja hapa**.

## 2. 0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

### 2.1 SARE ZA SHULE.

a) Suruali mbili za kaki zenye linda(kitambaa kaki namba moja)
*b)* Mashati mawili meupe ya mikono mirefu*.*
c) Sare za michezo kwa shule hii ni jezi rangi nyekundu(Full) moja na viatu vyamichezo.
d) Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi
e) Soksi jozi mbili nyeupe.
f) Mkanda wa kuvalia suruali ni mweusi wa ngozi.
g) Sweta yenye shingo V rangi ya bluu.
h) Track suti rangi ya kijani yenye ufito mweupe.
i) Nguo za kushindia (shamba dress) T-shirt rangi ya **njano(zito isiyo na maandishiwala michoro)** na suruari **dark blue** kitambaa kizito.
j) T-shirt **nyeupe** ( inapatikana jirani na shule kwa sh. 10,000/=)

### 2.2 MICHANGO YA SHULE

| NA | AINA YA MCHANGO | KIASI (Tsh) |
|---|---|---|
| 1 | Mchango wa uendeshaji wa shule | 55,000/- |
| 2 | Tahadhari | 5,000/- |
| 3 | Nembo | 5,000/- |
| 4 | Kitambulisho | 5,000/- |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**TANBIHI:** Michango yote ilipwe katika akaunti ya shule yenye nambari **60501100060** benki ya **NMB** kwa jina la akaunti: **NYERERE HIGH SCHOOL-MIGOLI.** (**Tafadhali andika jina la mwanafunzi kwenye pay in slip**).

### 2.3 MAHITAJI MENGINE MUHIMU :

i. Rimu za karatasi bunda 2 (kwa mwaka)
ii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika vimeambatanishwa.
iii. Scientific calculator kwa wanafunzi wenye tahasusi za EGM na HGE
iv. Godoro la sponji la DODOMA (2 ½ x 6) lenye ujazo wa nchi 3 ½
v. Mashuka pair 2 rangi ya pink na chandarua 1.
vi. Vyombo vya chakula (sahani,bakuli, kijiko na kikombe)
vii. Ndoo moja ya lita 20 na moja ya lita 10 zenye mifuniko.
viii. Tochi moja(ya kuchajiwa kwa jua) endapo kukiwa na tatizo la umeme.
ix. Kila mwanafunzi atapaswa kuja na water Squeezer moja na sabuni ya maji lita 5 kwa ajili ya usafi isipokuwa kwa **tahasusi ya EGM** wao watapaswa kuja na spedi ya chuma 1 kwa kila mmoja.
x. Mafaili mawili (2) ambayo ni flat ya plastiki.

## 3. MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE

i. Wizi
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/ utoro
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamiikwa ujumla
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtuyeyote yule
vi. Kufuga ndevu
vii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya
viii. Uvutaji sigara.
ix. Uasherati, ushoga, kuoa au kuolewa.
x. Kushiriki kutoa mimba
xi. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yaleyanayovunja sheria za nchi.
xii. Kusababisha mimba au kumpa mimba msichana
xiii. Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni
xiv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi au vifaa vinavyohusiana na simu ya mkononi kama laini chaja n.k katika mazingira ya shule(***kabla ya kufukuzwa shule mwanafunzi,mzazi/mlezi atatakiwa kulipa gharama za uharibifu wa miundombinu ya shule***)
xv. Kudharau bendera ya taifa na alama zingine za taifa
xvi. Kufanya jaribio la kujiua au kutishia kuua
xvii. Uharibifu wa mali za umma kwa makusudi

**TANBIHI ***

- Nguo za michezo zitatumika uwanjani tu na sio mazingira mengine ya shule.
- Nywele ni sehemu ya sare ya shule, zinatakiwa ziwe fupi za kuchana, aidha kuchaziwe fupi na safi wakati wote.
- Hairuhusiwi kuvaa bangili (kacha), au mapambo ya aina yoyote ile shuleni

**Mavazi ya aina nyingine nje ya haya yaliyotajwa hapo juu hayaruhusiwi kabisa shuleni, mwanafunzi atakaye pokelewa ni yule atakaye kuwa amevaa sare za shule zilizo ainishwahapo juu.**

**MWISHO**

Maagizo yote yatakaguliwa siku ya kuripoti shuleni. Mwanafunzi hatapokelewa endapo hatakuwa amekamilisha maagizo yaliyomo ndani ya fomu hii. Ukifika shuleni utasomewa tenasheria, kanuni na taratibu za shule hii. Ni wajibu wako kutii na kuzifuata kikamilifu. Ukikosa utaonywa kwa maandishi/mdomo au utaonywa kwa kupewa adhabu na ikilazimu utasimamishwa masomo kwa muda (suspension) au kufukuzwa shule kabisa ikibidi kwa mujibu wa sheria.

Mwisho kabisa nachukua nafasi hii tena kukukaribisha sana hapa **Nyerere High School- Migoli** na ni matarajio yangu kuwa ufikapo hapa utaitumia vema fursa hii muhimu uliyotunukiwa na Taifa lako kwani wengi wameikosa.

***Tafadhali mwanafunzi aje na mzazi/mlezi siku ya kusajiliwa hapa shuleni na kuhakikisha fomu zilizoambatanishwa na fomu hii zinajazwa kwa usahihi.***

**MERERE,O.E**
**MKUU WA SHULE**

**BAADHI YA VITABU AMBAVYO MWANAFUNZI ANAWEZA KUJINUNULIA KULINGANA NA TAHASUSI YAKE**

**VITABU VYA HISTORY:**

1. How Europe underdeveloped Africa by Walter Rodney.
2. Africa since 1800, 4th edition by Roland Olive and Atmore.
3. The political economy, imperialism by Nabudere.
4. Mastering Advanced level History book II by Kato.
5. World History Advanced Level by Samweli Mhajida.
6. Focus on modern world History History Advanced Level by Chakupewa.J etal (2012)paper I na Paper II.
7. Contemporary history events volume one first edition by Shibitali C.K
8. Major Events in the World History paper 2 Advanced Level Gervas.M Zombwe.

**VITABU VYA UCHUMI:**

1. Economic simplified East Africa Edition by N.A Saleem.
2. Ambilikile Advanced economic paper I.

**VITABU VYA GEOGRAPHY;**

1. Bunnett (2006) physical geography in diagram for Africa Longman Limited china.
2. Economic geography by Mogarn.
3. Human and economic geography by D.T Msabila.
4. The essential of practical geography Advanced level by Joseph William Njiku (2005).
5. Certificate of Human and economic Geography. By Morgan and Leong Chang.

**VITABU VYA KISWAHILI**

A. **USHAIRI:**
    1. Kimbunga - G.Gora (Taasisi ya uchunguzi wa Kiswahili) 1999.
    2. chungu Tamu-T.A Mvungu (Tanzania published house) 1985.
    3. Mapenzi bora-S.Robert (Mkuki na Nyota) 2003.
    4. Fungate ya Uhuru M.S Khatibu.

B. **RIWAYA;**
    1. Vuta n’ Kuvute- A.Shafi (Mkuki na Nyota)-1999.
    2. Kufikilika S.Robert-2003
    3. Mfadhili Hussein Tuwa.
    4. Usiku utakapokwisha-Mbunda Msokile-2007

C. **TAMTHILIA;**
    1. Moran -E.Mbogo
    2. Kivuli Kinaishi Said Mohamed-2007.
    3. Kwenye Ukingo wa Thim-E.Ussein
    4. Nguzo Mama-1982.

**ENLISH LANGUAGE**

1. New advanced level English by Charles. E
2. Advanced level English, A practical approach by Nicholous Asheli.
3. Advanced level literature by Nyambari Nyangwine.
4. Advanced level Learners Dictionary.
5. Teaching English as a foreign language by G.Broughton.
6. English form V and VII by M. Kadege.
7. Contemporary English for advanced level by Francis Mnyawe.
8. Complete course by M.Kadege.

**B-NOVEL:**

1. The beautiful ones are not yet born by A.K Amah.
2. A man of the people by C.Achebe.
3. Divine providence – Mkuki na Nyota.
4. Encounters from Africa – Macmillan.
5. The rape of the pearl-

Macmillan.C**-PLAYS/DRAMA;**

1. An Enemy of the people – H.Ibsen.
2. I Will Marry When I want-EAEP
3. Rwanda Magere by Okoti Omtatah-1991
4. The Pride – EAEP
5. Black Mamba-EAEP.

C**-POETRY;**

1. Selected poem from institute of education.
2. The wonderful Surgeon and other poem-Mkuki na Nyota.

**PURE MATHEMATICS;**

1. Pure mathematics I and II by J, K Backhouse.
2. Advanced level pure mathematics by Kinunda.
3. Advanced level pure mathematics by C.J Tranter- 2006
4. S.Chand mathematics for class XI, volume I and II by H.K DASS R.VERMA 2013
5. Calculator Casio.

**BASIC APPLIED MATHEMATICS (BAM):**

1. Basic applied mathematics for Advanced school form V and VI by Septine
2. Calculator (non programmable)

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAANYERERE**

**HIGH SCHOOL- MIGOLI**

**FOMU YA KUKUBALI NAFASI YA KIDATO CHA TANO**

(sehemu ya kwanza ya fomu hii ijazwe na mwanafunzi na sehemu ya pili ijazwe na mzazi ua mlezi)

| Picha |
|---|

## SEHEMU YA KWANZA

(sehemu hii ijazwe na nwanafunzi  mwenyewe)

Mimi___________________(mwanafunzi) kwa hiari yangu nakubali nafasi naahidi kutoshiriki/kuanzisha migomo, fujo na makosa ya jinai na nitafuata sheria zote za shule.

Jina la mwanafunzi____________________________________

Sahihi ya mwanafunzi______________

Tareh____/_____/201___

## SEHEMU YA PILI

(Sehemu hii ijazwe na mzazi/mlezi)

Mimi_____________________________mzazi/mlezi* wa ______________________________

Nakubali/ sikubali* nafasi aliyopewa mtoto wangu na kwamba muda wote awapo shuleni atalazimika kuwa mtii kwa walimu, wazazi, viongozi na jamii kwa ujumla. Atalazimika kufuata sheria zote zashule. Naahidi kuwa mwanangu atazifuata taratibu zote za shule hadi atakapo maliza shule.

Jina la mzazi/mlezi*_____________________________________

Sahihi ________________

Tarehe___/____/20____

***Futa isiyohusika**

**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAANYERERE**
**HIGH SCHOOL- MIGOLI**
**TAARIFA ZA MZAZI/MLEZI NA MWANAFUNZI**
(Fomu hii ijazwe na Mzazi/mlezi)

1. Jina kamili la Baba/ Mama/Mlezi*________________________________________
2. Mahusiano na wanafunzi(Baba/Mama/Mjomba n.k)________________________________
3. Namba ya kitambulisho cha NIDA_____________________________
4. Elimu yake _______________________________________________
5. Kazi yake ________________________________________________
6. Namba ya simu ___________________________________________
7. Anuani____________________________ Mji/mkoa___________________
8. Barua pepe _______________________________________________
9. Mahali anapoishi Mtaa/Kijiji____________________________Kata______________________
   Wilaya ________________________________ Mkoa________________________________
10. Wazazi wanaishi pamoja? NDIYO ☐ HAPANA ☐
11. Mtoto anaishi na BABA ☐ MAMA ☐ MLEZI ☐
12. Wazazi wote ni wazima? NDIYO ☐ HAPANA ☐ Kama Hapana, mzazi
    yupi amefariki?__________________________________________________
13. Tarehe ya kuzaliwa ya mwanafunzi _________________________________
14. Namba ya cheti cha kuzaliwa ______________________________________
15. Dini ya mzazi/mlezi*______________________________________________
16. Dhehebu _________________________________________________________
17. Anuani kamili ya sehemu ambako mtoto atakuwa anakwenda wakati wa likizo kama ni nje yaeneo ambalo mzazi/mlezi anakaa __________________________________
18. Mimi__________________________________________________mzazi/mlezi* wa
    ________________________________nakiri kuwa taarifa nilizozitoa hapo juu ni sahihi. Naahidi kushirikiana na walimu ili kuhakikisha kwamba kijana wangu anakuwa na tabia nzuri,mchapa kazi, na mwenye bidii.
    **NB:** ***Hakikisha unaambatanisha nakala ya cheti cha kuzaliwa cha mwanafunzi na kitambulisho cha* NIDA cha mzazi/mlezi kama kipo**

**PRESIDENT'S OFFICE**
**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**
**NYERERE HIGH SCHOOL –MIGOLI**

MEDICAL EXAMINATION FORM

**(To be completed by medical officer in respect with a new student)**

Full name________________________________

Age ____________________________________

1. Blood count (red and white)__________________________________________
2. Urine examination ________________________________________________
3. Stool examination ________________________________________________
4. Syphilis ________________________________________________________
5. T. B Test ________________________________________________________
6. Ear Test_________________________________________________________
7. Eye Test_________________________________________________________
8. Spleen _________________________________________________________
9. Abdomen _______________________________________________________
10. Additional information or any other physical, mental, hereditary of infectious diseases

______________________________________________________________________

Treatment after examination

______________________________________________________________________

**MEDICAL CERTIFICATE**

I certify that the above concerned has been examined and found **fit/not fit*** to pursuefor further education.

Signature______________

Designation________________________________________

Station ___________________________________________

(Official

stamp)Date__/_____/20___

**NB**. Fomu hii ijazwe na mganga katika hospitali inayotambulika na serikali **(sio zahanati)**

*Erase unwanted information